LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA YA MUDA WA UKOMO

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA YA MUDA WA UKOMO

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

SHUKRANI ........................................................................5
UTAMBULISHO.................................................................6
MAONO ...........................................................................6
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI ..........................................7
LENGO KUU.....................................................................7
DIBAJI .......................................................................... 8
1. Maana ya Ukomo wa Daawa ...................................... 10
2. Lengo la Ukomo wa Daawa ........................................ 10
3. Mwanzo wa Daawa.......................................................11
4. Upimaji wa Muda wa Daawa ......................................12
5. Maombi Kabla Ya Muda Wa Kawaida...........................13
6. Maombi Baada Ya Muda Wa Kawaida Kumalizika......14
7. Siku Zisizohusika Kwenye Ukomo Wa Daawa..............16
8. Ukomo Wa Daawa Katika Kukazia Hukumu ..................17
9. Ukomo Kwenye Shauri Lililokuwa Na Kizuizi ...................17
10.Maombi ya kupata Usajili wa Umiliki Kinzano..................18
11. Uwezo/Mamlaka ya Waziri Kuongeza Muda wa Ukomo wa Daawa .........................................................................19
12.Orodha Ya Baadhi Ya Madai Na Muda Wa Ukomo Wake........21
13.Ukomo wa Daawa kwenye Maombi ...............................22
14.Hitimisho ......................................................................24

# SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasharia wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi.  Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia,  Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET).
Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma yakusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pam oja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria am bayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.
Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au

maelekezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafahdhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## 1. MAANA YA UKOMO WA DAAWA

Neno ukomo limetumika kumaanisha muda ambao mdai katika jambo au shauri atafikia kikomo au mwisho wa kufanya madai hayo kwa mujibu wa sheria ya Ukomo wa Daawa, Sura ya 39 ya mabadiliko ya sheria ya mwaka 2002; kila dai au madai yana mwisho wake kisheria.

## 2. LENGO LA UKOMO WA DAAWA

Lengo la ukomo ni kuhakikisha kuwa mashauri yanafikia mwisho wake, maana milango ya madai haiwezi kufunguliwa milele. Lazima ufike wakati madai hayo yamalizike ama kwa malipo, maelewano au kulazimika kisheria kusamehe. Madai yanaweza kuwa kati ya mtu na mtu, mtu na mwajiri wake, mtu na shirika au kati ya shirika moja na jingine.

Pale linapotokea shauri la madai, mdai baada ya kutumia njia ya kawaida ya maelewano au usuluhishi bila mafanikio basi anaruhusiwa kupeleka madai yake mbele ya chombo cha sheria na katika muktadha huu chombo hiki ni mahakama au mabaraza ya usuluhishi. Katika kufanya hivyo kuna mipaka au vigezo vya lini au ni baada ya muda gani mdai anaweza kupeleka madai yake mbele ya chombo cha sheria ili haki ipate kutolewa.

## 3. MWANZO WA DAAWA

Neno daawa ni madai aliyo nayo mtu mmoja dhidi ya mwingine. Kwa mujibu wa sheria ya ukomo madai yoyote yale muda wake huanza kuhesabika tangu mgogoro wa kisheria unapoibuka baina ya pande mbili husika. Kwa mfano, katika madai yenye msingi kwenye ajira muda wa ukomo utaanza kuhesabika tangu tarehe ya kufukuzwa kazi.

## 4. UPIMAJI WA MUDA WA DAAWA

Mahakama chini ya sheria ya ukomo ya mwaka 1971 imepewa mamlaka ya kuongeza muda wa ukomo. Nyongeza ya muda chini ya sheria hii inahusu kukata rufaa nje ya muda wa kawaida katika shauri husika. Mahakama inatekeleza wajibu huu wa nyongeza ya muda wa kukata rufaa nje ya muda wa kukata rufaa kupitia maombi ya mdai au mrufani. Katika maombi hayo mwombaji anatakiwa atoe sababu na hoja za msingi za kuchelewa kukata rufaa ili ombi lake lipate kufikiriwa na hatimaye kukubaliwa na mahakama. Mahakama baada ya kupitia maombi hayo inaweza kuruhusu rufaa hiyo au kuitupilia mbali kama haioni hoja na sababu za msingi za kuchelewa kukata rufaa kwenye maombi ya mrufani.

## 5. MAOMBI KABLA YA MUDA WA KAWAIDA

Maombi ya aina hiyo yaweza kufanyika kabla ya muda wa kawaida wa kukata rufaa katika mazingira ambayo mwombaji anakuwa na jambo lisilokuwa la kawaida na kwa vyovyote vile haliepukiki.

Kwa mfano mtu anapokuwa mgonjwa na ikathibitishwa kwa vilelezo kutoka kwa daktari kuwa ni mgonjwa, katika hali kama hiyo maombi yanaweza kufanyika kabla ili hata mwombaji akifanya hivyo nje ya muda awe na kinga ya kisheria.

Mfano mwingine ni pale ambao mwombaji anatarajia kusafiri na ukomo wa kukata rufaa katika utaratibu wa kawaida utamalizika kabla ya yeye kurejea toka safarini. Katika hali kama hiyo anaweza kufanya maombi ya kukata rufaa kabla ya muda wa kawaida.

## 6. MAOMBI BAADA YA MUDA WA KAWAIDA KUMALIZIKA

Maombi ya namna hii ndiyo yamekuwa mengi zaidi kuliko aina ya mwanzo na ndiyo yamezoeleka. Mwombaji au mrufani huiomba mahakama ili imruhusu akate rufaa nje ya muda wa kawaida.

Shauri linapotolewa maamuzi na mahakama yenye mamlaka kisheria, maamuzi hayo hupokelewa kwa hali na namna tofauti miongoni mwa pande mbili yaani mdai na mdaiwa kutegemea na aliyeshinda au kushindwa shauri hilo au kwa yeyote ambae hakuridhika na maamuzi.

Ni haki kwa upande usioridhika na maamuzi husika kukata rufaa, haki hii ya kukata rufaa huwa inaelezwa kwenye hukumu ambapo muda maalumu wa kukata rufaa unakuwa umetolewa. Mfano shauri la ndoa likikamilika kukata rufaa kutoka mahakama ya wilaya kwenda Mahakamu kuu ni siku arobaini na tano (45). Hivyo basi panapotokea sababu

za msingi za kumfanya mrufani ashindwe kukata rufaa ndani ya muda wa kawaida haina budi afanye maombi ili mahakama imruhusu akate rufaa nje ya muda wa kawaida wa kukata rufaa.

Katika maombi hayo mwombaji hana budi kutoa sababu ni kwa nini ameshindwa kukata rufaa ndani ya muda wa kawaida. Baada ya mahakama kupitia maombi ya mwombaji na kuona kwamba kuna sababu za msingi za kuchelewa kwa mwombaji kukata rufaa basi itapitisha maombi yake na hivyo kumruhusu mwombaji kukata rufaa nje ya muda wa kawaida wa kukata rufaa.

Muhimu ieleweke kwamba mwombaji anapaswa kuandika barua ya kuomba nakala ya hukumu, tamko, tunu au uamuzi wa mahakama pale tu uamuzi au hukumu itaposomwa ili kumuwezesha kukata rufaa.

## 7. SIKU ZISIZOHUSIKA KWENYE UKOMO WA DAAWA

Katika kuhesabu ukomo wa daawa wa baadhi ya madai, kuna siku hazihusishwi/ hazihesabiwi kwenye ukomo. Siku hizo ni:-

- Siku ya kupeleka maombi ya kukata rufaa.
- Siku ya kupeleka maombi ya kufanya marejeo
- Siku ambapo hukumu inayolalamikiwa ilipotolewa.
- Muda wote tokea hukumu iliposomwa hadi kupatikana kwa nakala ya hukumu ili kukuwezesha kukata rufaa.

## 8. UKOMO WA DAAWA KATIKA KUKAZIA HUKUMU

Katika suala zima la maombi ya kukazia hukumu, muda ambao mdaiwa atakuwa nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hautahesabika kwenye ukomo.

## 9. UKOMO KWENYE SHAURI LILILOKUWA NA KIZUIZI

Pale mahakama inapokubali maombi ya kizuizi, muda wote ambao kizuizi kitafanya kazi hautahesabika kwenye ukomo. Maombi ya kizuizi ni maombi yanayoletwa mahakamani kuomba mtu azuiwe kufanya jambo fulani, mfano maombi ya kizuizi mtu asijenge au kulima kwenye eneo fulani lenye mgogoro.

Vile vile iwapo mtu ana uhalali wa madai katika shauri fulani na inatokea mtu huyo anafariki kabla ya muda wa madai yake kuisha, muda wa ukomo utaanza kuhesabika ndani ya mwaka mmoja baada ya kifo chake. Ili kuwapa wafiwa nafasi ya kuteua msimamizi wa mirathi ili aweze kufuatilia madai hayo kwa manufaa ya wale waliokuwa wanamtegemea kama mke, mume au watoto.

## 10. MAOMBI YA KUPATA USAJILI WA UMILIKI KINZANO

Ikiwa mtu atakuwa na madai juu ya ardhi inayomilikiwa chini ya umiliki mkinzano, basi mtu huyo anaweza kuomba mahakama kuu itoe tamko kwamba mtu huyo asajiliwe kama mmiliki wa ardhi hiyo. Mahakama Kuu baada ya kujiridhisha na pia kupitia maombi ya mwombaji itatoa tamko kwamba mwomaji ndiye asajiliwe kama mmiliki wa sehemu husika.

Ifahamike kuwa mtu hawezi kupata umiliki kinzano katika ardhi ya umma. Hakuna shauri lolote au mwenendo wowote wa madai ya ardhi kwa niaba ya serikali ya Jamhuri ya Muungano au Rais yatakayotupiliwa mbali kwa kigezo cha kuisha muda wake wa ukomo.

## 11. UWEZO/MAMLAKA YA WAZIRI KUONGEZA MUDA WA UKOMO WA DAAWA

Kulingana na sheria ya ukomo sura ya 89, Waziri anayehusika na masuala ya Sheria amepewa mamlaka ya kuongeza muda kwenye madai mbalimbali yaliyofikia ukomo ikiwa mhusika ataomba na kutoa sababu za msingi za kuchelewa kufungua shauri ndani ya muda. Waziri atafanya hivyo pale atakapoona kuwa kufanya hivyo kutaleta haki na usawa na atatoa ruhusa hiyo baada ya kuwasiliana na mwanasheria mkuu wa serikali kwa maandishi yaliyosainiwa.

Sheria hii inampa Waziri ruhusa ya kuongeza si zaidi ya nusu ya muda wa ukomo wa madai husika. Kwa mfano katika madai ya kupata malimbikizo ya kodi, muda wa ukomo ni miaka sita, hivyo basi uwezo wa Waziri wa kuongeza muda wa ukomo katika madai ya namna hii si zaidi ya miaka mitatu. Kwa msingi huo basi, Waziri amepewa mamlaka ya kuongeza muda ambao si zaidi ya nusu ya muda wa ukomo unaotolewa kulingana na sheria husika.

## 12. ORODHA YA BAADHI YA MADAI NA MUDA WA UKOMO WAKE

» Madai ya fidia kwa kufanya au kuacha kutimiza wajibu ipasavyo kisheria ukomo wake ni mwaka mmoja (1);
» Madai ya kurejeshewa mali iliyochukuliwa, ukomo wake ni miaka miwili (2);
» Madai ya kurejeshewa pesa za michango, ukomo wake ni miaka miwili (2);
» Madai ya kutupilia mbali mauzo ya mali kwa ajili ya kukazia hukumu, ukomo wake ni miaka miwili (2);
» Madai yenye msingi kwenye sheria ya madhara, ukomo wake ni miaka mitatu (3);
» Madai ya kwenye mikataba ambayo hayajawekwa bayana kulingana na sheria husika, ukomo wake ni miaka sita (6);
» Madai ya kupata malimbikizo ya kodi, ukomo wake ni miaka sita (6);

- Madai yenye msingi kwenye hukumu ukomo wake ni miaka sita (6);
- Madai ya kurejeshewa ardhi, ukomo wake ni miaka kumi na miwili (12);
- Madai ya kupata mali ya marehemu inayohamishika, ukomo wake ni miaka kumi na miwili (2);
- Madai ya serikali au kwa niaba ya serikali, ukomo wake ni miaka sita (6).

## 13. UKOMO WA DAAWA KWENYE MAOMBI

- Maombi ya kutupilia mbali maamuzi, hukumu au tunu ya mahakama, ukomo wake ni siku thelathini (30);
- Maombi ya marejeo au mapitio ya hukumu ukomo wake ni siku thelathini (30);
- Maombi ya kutuipiliwa mbali maamuzi ya kufuta dai mahakamani, ukomo wake ni siku thelathini (30);

- Maombi ya kutupilia mbali maamuzi ya dai lililosikilizwa upande mmoja, ukomo wake ni siku thelathini (30);
- Maombi ya utenguzi wa uuzaji wa mali uliofanyika ili kukazia hukumu, ukomo wake ni siku thelathini (30);
- Maombi ya kurejesha dai au shauri lililotupiliwa mbali kwa kutoonekana mdai mahakamani, ukomo wake ni simu arobaini na tano (45);
- Maombi ya kusikilizwa tena kwa rufaa iliyosikilizwa upande mmoja, ukomo wake ni siku thelathini (30);
- Maombi ya kukazia hukumu ya mahakama ambapo muda maalumu wa ukomo wa daawa husika haujatolewa na sheria yoyote, ile miaka kumi na miwili (12);
- Maombi yoyote yale ambayo ukomo wake haujatolewa chini ya sheria yoyote ile, ni miaka sita (6);

## 14. HITIMISHO

Katika kitini hiki tumeweza kujifunza mambo mbalimbali kama vile malengo ya sheria ya ukomo wa daawa, maana na mwanzo wa daawa, upimaji wa muda wa daawa, maombi kabla ya muda wa kawaida wa kaawa kuisha, maombi baada ya muda kuisha, siku zisizohusika kwenye ukomo wa daawa, ukomo wa daawa katika mambo mbalimbali, uwezo wa Waziri kuongeza muda wa ukomo wa daawa, ukomo wa baadhi ya madai kwenye sheria mbalimbali na ukomo wa daawa kwenye maombi mbalimbali.

Ndugu msomaji ni matumaini yetu kuwa kitini hiki kimekupa ufahamu kuhusu muda wa kufungua madai ya daawa mahakamani na kwenye mabaraza mbalimbali ili kuweza kupata haki yako. Hii itakusaidia wewe binafsi, pia itakuwezesha kushauri watu wengine kuhusu ufunguaji wa madai yao mahakamani ndani ya muda uliopangwa kisheria.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva,
Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*